**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# NGARA HIGH SCHOOL MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**Namba za Simu…………………..**

**Mkuu wa Shule:0784616865**

**Makamu Mkuu wa Shule:0756886787**

**Matron/Patron…0743530060**

**Shule ya Sekondari:NGARA HIGH SCHOOL**

**S.L.P.. 60**

**Tarehe......30.3. 2024**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**……………………………………………….**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI NGARA HIGH SCHOOL HALMASHAURI YA NGARA MKOA KAGERA MWAKA 2024**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka na atasoma tahasusi ya **HGL** na **HKL**

Shule ya Sekondari **NGARA HIGH SCHOOL** ipo umbali wa Kilometa ……33… Kaskazini/Kusini/Mashariki/Magharibi mwa Mji wa **NGARA** Usafiri wa basi kutoka mjini …… unapatikana katika kituo cha mabasi **BENAKO** Nauli ni **Shilingi 3,000** kwa pikipiki na Shilingi ......................kwa bajaji.

Muhula wa Masomo unaanza 1.7.2024 hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 15.7.2024 Mwisho wa kuripoti ni tarehe **31/7/2024**

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 Sare za Shule**

*i.* Sare ya shule hii ni **Suruali nyeusi** kwa Wavulana (*Size 15chini yenye mfuko mmoja nyuma)isiwe modo zingatia.*
ii. Mashati Mawili (*Rangi nyeupe mikono mirefu*);
*iii.* Sare ya Michezo ni Track suit za nyeusi na tshirt kwa wavulana (*Pair moja moja).tangu sàwa na track suit iwe ni nyeusi.*
iv. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;
v. Soksi jozi mbili nyeusi za shule;
vi. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali;
vii. Sweta ugoro
viii. Nguo za kushindia (*shamba dress*) suruali moja (Dark bluu.
ix. Tisheti (T-shirt) moja.(inapatikana shuleni )

**2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari Nane (8) Counter book 4 Quire
ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika .

**iv.** Godoro ni 2¹/²/6 kwa wanafunzi (lin**apatkana shuleni kwa bei ya ya sokoni).**
*v.* Mashuka Jozi 2, rangi ya Bluu bahari.,blanket 1, tangu yoyote . chandarua 1 . Shuka(*rangi ya Bluu bahari*
vi. Nguo za ndani

vii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe vya bati siyo contena)
viii. Ndoo 1 ndogo (lita Kumi) yenye mifuniko;
ix. jembe 1, siko1, mifagio 2 wa ndani na nje.Lita 5 sabuni ya maji (chooni)

## 2.3 Michango mbalimbali

**a) Shule za Bweni**

| **Na** | **Jinala ac.Ngara highschool** | **Aina ya Mchango. Ac no.32110021916 .** | **Kiasi** |
|---|---|---|---|
| 1. | | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | | Nembo | 5,000/= |
| 5. | | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | | **Jumla** | **80,000/=** |

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;

iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba auUgonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;

vi. Kufuga ndevu;
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
viii. Uvutaji wa sigara;
ix. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;

x. Kusababisha mimba;
xi. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiii. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xiv. Kudharau Bendera ya Taifa;
xv. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xvi. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule ……………………………………………**

**Jina la Mkuu wa Shule .ABEL ELIABU…………………………….**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule ………………………………..**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu nakuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule: 0753099624/0784616865**
- **Makamu Mkuu wa Shule:0756886787**
- **Mwandamizi Taaluma: 0768223210**
- **Mwandamizi Malezi 0743530060**

**FOMU HII IJAZWE NA IREJESHWE SHULENI**

**Mimi (Jina la Mwanafunzi) ………………………………………………… naahidi kuwa**

**mtiifu wa sheria na kanuni zote za shule. Sitashiriki katika vitendo viovu kwa muda wote nitakao**

**kuwa shuleni kwa mfano: kumiki simu shule, kushiki kwenye migomo, fujo, makosa ya jinai n.k.**

**Sahihi …………………………………… (Mwanafunzi) Tarehe …………………………**

**Mimi (Jina la Mzazi/mlezi) ……...……………...……………………………………………….**

**Mzazi/Mlezi wa............................................................................................ nakiri kusoma maelekezo na**

**masharti yote ya shule, nakubaliana na sheria, kanuni, taratibu, michango na maelekezo mengine**

**yatakayotolewa na shule.**

**Sahihi ………………… (Mzazi/mlezi) Simu .................................Tarehe …………………...**

**Namba za simu na picha za wazazi/walezi**

**(i) Jina ………………………………… No. Simu...............................Uhusiano ……………**

**PICHA YA**

**MZAZI/MLEZI**

**TAJWA**

**(ii) Jina ………………………………… No. Simu...............................Uhusiano ……………**

**PICHA YA**

**MZAZI/MLEZI**

**TAJWA**

**(iii) Jina… ............................................. No. Simu……………………...Uhusiano………….**

**PICHA YA**

**MZAZI/MLEZI**

**TAJWA**

**MEDICAL CERTIFICATE**

**DATE …………………**

**STUDENT'S NAME ……………………………………….……………………….**

**(NAME IN FULL)**

**THE MEDICAL OFFICER:**

**………………………………………….**

**…………………………………………..**

**…………………………………………..**

**I have examined the above named student and consider him/her physically and**

**mentally fit for his/her studies. The examination has included the following categories:**

**a) Eye – sight ……………………………………………………….…………...**

**b) Hearing ………………………………………………………….….……….**

**c) Limbs ………………………………………………………….……….**

**d) Venereal diseases …………………………………………………..…...**

**e) Epilepsy …………………………………………………….…………**

**f) Leprosy …………………………………………………………...….**

**g) Neuroses ……………………………………………………………….**

**h) Other serious Diseases ……………………………………………….**

**i) Pregnancy ……………………………………………………………**

**Date ………………………………………………… Signature …………………………**

**Station ……………………………………………… Designation ………………………**